**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Sita – Tarehe 16 Septemba, 2026**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. KIAPO CHA UAMINIFU

**Mhe. Nassor Ahmed Mazrui**

**Mhe. Omar Said Shaaban**

## II. TAARIFA YA SPIKA:

## III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo:**

Hotuba ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024.

## IV. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

28. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Serikali imetunga Sheria ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa) Namba 6/2022 ambayo imetaja fursa mbalimbali za Wajumbe wakati wa utumishi wao, lakini haijaeleza chochote kuhusu Wajumbe Wawakilishi wanapomaliza muda wao wa kuwatumikia wananachi katika kipindi cha miaka mitano.

(a) Je, kuna mpango gani wa kuanzisha skimu maalumu ya mafao endelevu kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaomaliza muda wao ambao baadhi yao hali zao za maisha zinapata changamoto.

(b) Kwa kiasi gani Ofisi ya Makamu wa Pili ipo tayari kushirikiana na Afisi ya Baraza la Wawakilishi, kufanya utafiti katika mabunge mbalimbali ulimwenguni kujifunza mipango ya kuwahudumia Wabunge wanaomaliza muda wao.

(c) Kwa hivi sasa, kuna mpango gani wa dharura unaoweza kuanzishwa na Serikali ili kuwasaidia Wajumbe waliomaliza muda wao ambao hali zao za maisha na kiafya zipo duni.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

190. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Mabaraza ya Wilaya ya Watu Wenye Ulemavu yana mchango mkubwa katika kutambua na kushughulikia changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu katika ngazi ya jamii.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyapatia usafiri mabaraza haya, ili kufanikisha ufuatiliaji wa watu wenye ulemavu.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

216. MHESHIMIWA MOHAMMED MANZI HAJI (Jimbo la Mwanakwereke) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika Wilaya ya Magharibi 'B' kuna maeneo yenye ongezeko kubwa la watu na shughuli za biashara zinazopelekea uwepo wa changamoto ya uzalishaji mkubwa wa taka.

(a) Je, Serikali imeweka mkakati gani wa Mpango wa Usimamizi wa Taka (Waste Management Plan), wenye kuonesha kiasi cha taka kinachozalishwa, kinachokusanywa, gharama kwa tani na eneo la mwisho la kutupa taka.

(b) Kwanini Serikali haioni haja na umuhimu wa kuzichakata taka kwa kuzalisha bidhaa nyengine mpya, ili kupunguza uchafuzi wa mazingira na kupunguza kiwango cha taka kinachopelekwa katika jaa kubwa.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

49. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Licha ya wananchi wa Zanzibar kutumia mbinu tofauti za kujinasua na mfumko wa bei ambao kila siku unaathiri uchumi wao.

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha thamani ya fedha inalindwa na uchumi unakuwa imara.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

155. MHESHIMIWA MOZA MOHAMMED KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Ili mtu aweze kuwa na afya bora anahitaji kupata maji safi na Salama. Hata hivyo, katika Mtaa wa Mapinduzi Mjini, Mkoani, Kinyasini, Mbuguni na Uweleni, wananchi wa mitaa hiyo wanapata maradhi ya mripuko kama matumbo ya kuharisha na kipindupindu kwa sababu kubwa ya kupasuka kwa bomba za maji na kusababisha uchafuzi wa maji hayo.

Kwanini Serikali haibadilishi miundombinu ya maji ya maeneo hayo, ili kupuguza tatizo hili sugu la maradhi ya mripuko na kuwalinda wananchi dhidi ya maradhi.

268. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa Wilaya ya Mkoani imebarikiwa kuwa na mali asili kwa wingi kama vile mawe, kifusi na kokoto.

Je, kwa kiasi gani Baraza la Mji Mkoani linafaidika na matumizi ya rasilimali hizo.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

229. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Naipongeza Serikali katika jitihada zake za ujenzi wa viwanja na skuli za ghorofa katika maeneo mbalimbali ndani ya jimbo la Fuoni. Viwanja ambavyo vitatoa mchango mkubwa kwa wanamichezo ikiwa ni pamoja na wanafunzi.

Kwanini Serikali haioni haja ya kujenga viwanja vya michezo katika maeneo yale yanayojengwa skuli ambayo yana nafasi ya ujenzi wa kiwanja hususan Skuli ya Mambosasa na Kibondeni.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

170. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa tatizo la ufinyu wa madarasa ya kusomea unazidi kuwa kikwazo katika Skuli ya Sekondari ya Uzalendo.

(a) Je, kwa kiwango gani Serikali inafahamu kuwa Skuli ya Sekondari ya Uzalendo ina ufinyu wa madarasa.

(b) Je, lini wananchi wanaotumia eneo hilo watarajie kujengewa skuli yenye uwezo wa kukidhi haja, ili kuepukana na mrundikano wa wanafunzi madarasani.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

12. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Bandari ya Wesha imekua ndio bandari pekee kwa Kisiwa cha Pemba inayotumika kwa kuingizia nishati ya mafuta.

(a) Je, Serikali imechukua jitihada gani kuboresha bandari hiyo kwa kuweka miundombinu bora.

(b) Ni upi mpango wa Serikali wa kupatikana kwa bandari ya kisasa ya kushushia mafuta Wesha.

101. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Bado kuna changamoto ya usafiri wa ndege kwenda na kurudi Kisiwani Pemba.

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya kusaidia kumaliza changamoto hii ambayo imeendelea kwa muda mrefu sasa.

(b) Je, Serikali ina mkakati wa kutumia ndege za Shirika la Ndege la Tanzania, ili iweze kuongeza safari za kwenda na kurudi kisiwani Pemba.

271. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa kuwa Serikali haina mpango wa kuwalipa fidia wananchi walioharibiwa vipando vyao wakati wakipisha ujenzi wa barabara unaoendelea hapa nchini. Na kwa kuwa hakuna uhakiki wala tathmini iliyofanyika kabla ya ujenzi wa barabara hizo kuanza kujengwa.

Ni lini Serikali itawapimia wananchi waliopitiwa na barabara hizo, ili wajue mipaka na ukomo wao wa kutumia ardhi, ili kuepusha usumbufu kwa siku za baadae.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

42. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ufugaji wa wanyama ni miongoni mwa shughuli muhimu za kiuchumi kwa wananchi wa Zanzibar. Hata hivyo, mifugo inakabiliwa na maradhi yanayohitaji chanjo za wakati na zenye ubora.

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuhakikisha wafugaji wanapata chanjo bora na kwa wakati, ili kulinda mifugo na kuimarisha Sekta ya Ufugaji.

221. MHESHIMIWA JABU MAKAME JUMA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali ilikuwa inamiliki maghala ya akiba ya chakula katika maeneo ya Saateni, maghala ambayo hivi sasa hayafahamiki kama bado yanaendelea kumilikiwa na Serikali au watu binafsi.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na maghala ya akiba, ili kuhifadhi chakula cha kutosha.

(d) Je, maghala ya Saateni kwa hivi sasa yanamilikiwa na nani, na Serikali inapata kiwango gani cha fedha kwa mwaka.

**Wizara ya Afya:**

238. MHESHIMIWA MARYAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha Afya Mgelema kinakabiliwa na upungufu wa watumishi. Changamoto hii imekua kubwa katika kipindi cha nyakati za usiku kutokana na umuhimu wa huduma za afya kwa wananchi, hasa wagonjwa wa dharura.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza idadi ya madaktari na watumishi wa afya katika kituo cha afya Mgelema, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora saa zote.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

282. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Wakulima wa mwani wameendelea kulalamikia bei ndogo ya zao hilo kwa kipindi kirefu, licha ya kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na maisha.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha bei, ili kuongeza kipato cha wakulima wa mwani.

(b) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa na Serikali katika kuongeza thamani na uchakataji wa zao la mwani hapa Zanzibar.

(c) Je, Serikali inawahakikishia vipi wakulima wa mwani kunufaika ipasavyo na mnyororo mzima wa thamani ya zao hilo.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

138. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Kuwa na nambari nyingi za utambulisho kama vile Kadi ya Mzanzibari Mkaazi (*ZANID*), Kadi ya Mwanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*), Kadi ya Mpiga Kura (*Voter* ID), Bima ya Afya, leseni na kadhalika, husababisha mgawanyiko wa utambulisho (identity *fragmentation*). Mgawanyiko huu huleta vikwazo vikubwa katika mageuzi ya kidijitali, mifumo kusomana na hata *cashless economy*.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuandaa Sera ya Mfumo wa *unique identification number* kwa raia wote wa Zanzibar, ili kurahisisha utoaji wa huduma za kidijitali.

## V. <u>HOJA ZA KAMATI:</u>

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo:**

Hotuba ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024.

**Zanzibar,**
**16 Septemba, 2026.**

**(Ramadhan Khamis Juma)**
**KAIMU KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**